

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania linawaalika wadau kutoa maoni kuhusu Maazimio yaliyowasilishwa na Serikali kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge katika Mkutano wa Kumi na saba (17) unaoendelea Jijini Dodoma.

Aidha, Bunge pia linawaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7), Bill, 2019*]. Maazimio hayo na Muswada vimeelekezwa kwenye Kamati zifuatazo;-

Mosi, Tarehe 7 Novemba, 2019, Kamati ya Nishati na Madini itapokea maoni ya Wadau kuhusu Azimio la Kuridhia kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua (*Framework Agreement on the Establishment of the International Solar Alliance – ISA*).

Kikao cha kupokea maoni ya wadau kuhusu Azimio hili kimepangwa kufanyika saa 7:00 Mchana, katika Ukumbi wa Msekwa C uliopo katika Ofisi Kuu ya Bunge Dodoma.

Pili, Tarehe 8 Novemba, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira itapokea maoni ya Wadau kuhusu Maazimio matatu yafuatavyo;-

- i) Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (*Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*);
- ii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu (*The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development*); na

- iii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (*Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization – WTO*).

Vikao vya kupokea maoni ya wadau kuhusu Maazimio hayo vimepangwa kufanyika kuanzia saa 5:00 Asubuhi katika Ukumbi Na. 49 uliopo katika Jengo la Utawala Annex - Ofisi Kuu ya Bunge Dodoma.

Tatu, Tarehe 8 Novemba, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu itapokea maoni ya Wadau kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (EAC Protocol on ICT Networks).

Kikao cha kupokea maoni ya wadau kuhusu Azimio hilo kimepangwa kufanyika saa 7:00 Mchana katika Ukumbi Na. 38 uliopo katika Jengo la Utawala Annex - Ofisi Kuu ya Bunge Dodoma.

Nne, Tarehe 9 Septemba, 2019 Kamati ya Katiba na Sheria itapokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.7) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7), Bill, 2019*],

Kikao cha kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada huu kimepangwa kufanyika saa 7:00 Mchana katika Ukumbi wa Msekwa - Ofisi Kuu ya Bunge Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Maazimio hayo, Kamati inawaalika wadau wote kufika na kuwasilisha maoni yao kabla Maazimio hayo hayajapelekwa katika hatua nyingine.

Maoni ya wadau pia yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya Posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

Barua pepe: cna@bunge.go.tz

Muswada na Maazimio haya yanaweza kupakuliwa kupitia tovuti ya Bunge ya www.parliament.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

06 Novemba, 2019.